

MAKUENI BOYS HIGH SCHOOL

KISWAHILI KIDATO CHA NNE APRIL HOLIDAY ASSIGNMENT 2020

Maswali ya Jumla ya Kudurusu

Maswali ya Mukhtadha

1. “Limekabwa shingoni na tai ya buluu iliyo zama kwenye misuli ya shingo fupi nene.”
 - a) Fafanua mukhtadha wa maneno haya. (al.4)
 - b) Eleza mbinu tatu zilizotumiwa katika dondoo hili. (al.6)
 - c) Eleza jazanda inayojitokeza katika hadithi hii. (al.6)

2. “Ninatupa macho huku na kule”
 - a) Yaweke maneno haya katika mukhtadha wake. (al.4)
 - b) Eleza sifa za anayetupa macho. (al.8)
 - c) Fafanua mbinu moja inayotumiwa katika dondoo hili. (al.2)
 - d) Fafanua maudhui yoyote matatu yanayojengwa na huyu anayetupa macho. (al.6)

3. “Yaani tabia ya kata na kupiga mbizi mtungini.”
 - a) Eleza mukhtadha wa maneno haya. (al.4)
 - b) Eleza mtindo uliotumiwa katika dondoo hili. (al.4)
 - c) Jadili kikamilifu jinsi kata inavyopiga mbizi mtungini kwa kurejelea hadithi husika. (al.4)

4. “Asingekubali kamwe kupata mji, umeme, matibabu na huduma zote za msingi buru huku mwananchi asiye na hata upumzi wa kuinuka alipo kwa dhiki na ufukara akilazimika kulipia yote.”
 - a) Uweke usemi huu katika mukhtadha wake. (al.4)
 - b) Fafanua maudhui yoyote manne yanayojitokeza katika dondoo hili. (al.8)
 - c) Eleza sifa za anayerejelewa na usemi huu. (al.4)
 - d) Ana umuhimu gani anayerejelewa na dondoo hili. (al.4)

5. “Hapo tena ilimjia ile picha chafu ambayo haijabanduka mpaka leo tokeo wakati ule ilipoanza.”
 - a) Yaweke maneno haya katika mukhtadha wake. (al.4)
 - b) Fafanua tamthilia za usemi mbili zilizotumiwa katika dondoo hili. (al.4)
 - c) Ni picha chafu chafu gani hii? (al.2)
 - d) Fafanua maudhui yoyote manne yanayojengwa na anayerejelewa na usemi huu. (al.10)

6. “ Mimi nimepika leo, na wewe ni juu yako kuondosha vyombo juu ya meza na kuviosha aui kuvitia vyakula vilivyobaki ndani ya friji.”

- a) Eleza mukhtadha wa maneno hay. (al.4)
- b) Huku ukitoa mfano, fafania mbinu iliyotumiwa katika dondoo hili. (al.2)
- c) Onyesha jinsi usasa unavyojitokeza katika hadithi inayorejelewa na mukhtadha huu. (al.14)

Maswali au Insha

1. “Viongozi wa Kiafrika wamefeli pakubwa katika harakati zao za uongozi.” Tetea kauli hii kwa kurejelea hadithi fupi za ‘Tumbo Lisiloshiba,’ ‘Shibe Inatumaliza’ na ‘makubwa.’
2. Kwa kurejelea hadithi zozote tano, jadili changamoto zinazokumba sekta ya elimu katika mataifa mengi barani Afrika. (al.20)
3. “Kiona nyuma ni mbinuy ambayo imetawala hadithi nyingi za diwani ya *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*,”. Tetea kauli hii kwa kurejelea hadithi zozote sita.
4. “Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi.” Unga mkono usemi huu kwa kuutolea mifano maridhawa kutoka katika hadithi zozote saba kutoka katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. (al.20)
5. Kwa kurejelea hadithi zozote nane katika diwani ya *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi nyingine*, onyesha nafasi ya mwanamke kataika jamii. (al.20)
6. “ Kinaya ni mtindo ambao umejitokeza katika hadithi zote za diwani hii.” Jadili kwa kurejelea hadithi zozote kumi. (al.20)

FASIHI

1. Tathmini mchango wa ukabila katika kuivunja jamii ya wahafidhina. (al.20)
2. Kwa kurejelea Tamthilia ya Kigogo, Jadili mbinu ishi unazojifunza kutokana na Tunu. (al.20)